**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA OFISI YA RAIS - TAMISEMI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

Shule ya Sekondari Mlangali
SLP 535
MBOZI - SONGWE,
TAREHE ………..

Kumb Na: MLSS/ADM/2022/02
Mzazi / Mlezi wa Mwanafunzi ………………
S.L.P ………………………………………...
……………………………………………....

**YAH: MAELEZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MLANGALI HALMASHAURI YAWILAYA MBOZI MKOA WA SONGWE MWAKA 2022/ 2023**

Nafurahi kukutaarifu kuwa mwanao amechaguliwa kujiunga na Kidato cha Tano katika Shule hii mwaka 2022/23 tahasusi ya PCB/PCM. Shule ya Sekondari MLANGALI ipo umbali wa Kilometa 32 kutoka stendi kuu ya mji wa VWAWA na kilometa 12 toka mji mdogo wa MLOWO. Usafiri wa Bajaji, Noa na Bodaboda kutoka stendi ya mlowo unapatikana ni shilingi 1500/= tu kwa Noa na Bajaji na shilingi 4000/= kwa bodaboda mpaka shuleni. Ili kufika kirahisi shuleni nashauri teremka kituo cha mabasi mji mdogo wa Mlowo utapata usafiri kirahisi mpaka shuleni.

Muhula wa masomo unaanza tarehe 05/09/2022 Hivyo mwanafunzi anatakiwa kuripoti shuleni kuanzia tarehe 03/09/2022. Mwisho wa kuripoti ni tarehe 04/09/2022.

Tunakupongeza wewe pamoja na wazazi/walezi wako kwa kufikia hatua hii. Tunatumaini kuwa utaitumia nafasi hii adimu kujielimisha zaidi na kujiwekea msingi wa maisha bora wewe mwenyewe, jamii na taifa kwa ujumla.

Kwa muda wote wa masomo ya Kidato cha V na VI, utatakiwa kutoa ushirikiano wa kutosha kwa walimu na walezi wako shuleni. Utatakiwa kuwa na tabia njema na kulinda heshima yako na ya shule yako utakapokuwa nje ya shule au likizoni, Kinyume cha hayo unaweza kupoteza nafasi hii kwa sababu za utovu wa nidhamu.

## 2.1 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA:-

## SARE YA SHULE

Sare ya shule hii ni suruali mbili moja ya rangi ya khaki na nyingine rangi nyeusi. Suruali mshono wa modo au jinsi/kubana haikubaliki kabisa hapa shuleni. Zinagatia maelekezo ya kila sare hapo chini;


**(a) Suruali**

- Upana wa mkanda wa suruali kiuno uwe inchi 2
- Iwe na mifuko mitatu (3) (miwili pembeni ya kutoboa na mmoja nyuma upande wa kulia).
- Upana wa suruali chini uwe inchi 17 (Si kinyume na hapo).
- Suruali iwe na turn up na marinda mawili.

Rangi za vitambaa vya suruali zimeambatanishwa hapo chini.



**Suruali ya Khaki**



**Suruali ya Nyeusi**

**(b) Shati**


Uje na shati mbili nyeupe za mikono mirefu, aina ya tetron, shati liwe na mfuko mmoja upande wa kushoto.

**(c) Sweta**

Uje na sweta moja rangi ya kijani kibichi na moja rangi damu ya mzee.



**Sweta Rangi ya Kijani kibichi**



**Sweta Rangi ya Damu ya Mzee**

- Uje na Viatu vya ngozi rangi nyeusi vya kufunga na kamba (gidamu) vyenye kisigino kifupi.
- Uje na Mkanda wa suruali mweusi wa ngozi.
- Uje na soksi ndefu rangi nyeusi pea mbili kwa ajili ya shule.
- Nguo za kuvaa nje ya darasani (shamba dress) ni T-shirt ya bluu shingo ya mviringo na suruali damu ya mzee (mashariti ya suruari kama yalivyo kifungu (a) ).

**(d) Sare za Michezo**

- Uje na Track suit rangi nyeusi tepe nyeupe



- Uje na Raba/"njumu" jozi moja na Soksi ndefu rangi ya bluu kwaa ajili ya Michezo.

**(e) Vifaa vya Malazi**

(i) Uje na mashuka mawili rangi ya pinki.
(ii) Uje na neti moja kwa ajili ya mbu.
(iii) Uje na blanketi zito moja rangi yeyote, hali ya Mlangali ni Baridi.
(iv) Uje na godoro futi 2.5 na mto 1.
(v) Uje na taulo la kuogea.

**(f) Vifaa vya Darasani**

(i) Non-Programmable Scientific calculator 1 f:x 991,dissecting set kwa waliochaguliwa tahasusi ya PCB (kabidhi kwa mtaalamu wa maabara ufikapo shuleni)
(ii) Daftari kubwa 10 (counter books Quire 4), kalamu za wino nyeusi/blue, Mathematical set (mkebe), Vitabu mbalimbali vya masomo kulingana na mchepuo wako. Kitabu ni mali ya mwanafunzi.

**(g) Vifaa vya Chakula, Usafi na Kazi**

(i) Jembe 1 lenye mpini aina ya fosholo, panga 1, na kwanja 1.
(ii) Ndoo moja lita 20 na moja lita 10, sahani moja, bakuli moja, kikombe kimoja na kijiko kimoja na sanduku la chuma moja lenye kufuli (trunker)
(iii) Vifaa vya usafi hard broom 1, soft broom 1, mopa 1 na mfagio aina ya chelewa 1.

## 2.2. ADA NA MICHANGO YA SHULE

a) **Ada ya Shule** kwa mwaka ni shilingi **70,000**/= .Unaweza kulipa kiasi cha shilingi **35,000** kwa muhula au kulipa ada yote kwa mara moja.

b) **Michango inayotakiwa kulipwa na mzazi/mlezi ni:-**

(i) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya ukarabati wa samani
(ii) Shilingi 6,000/= kwa ajili ya kitambulisho na picha
(iii) Shilingi 20,000/= kwa ajili ya taaluma
(iv) Shilingi 30,000 /= kwa ajili ya wapishi, walinzi na vibarua wengine
(v) Shilingi 2,000/= nembo ya shule
(vi) Shilingi 10,000/= kwa ajili ya huduma ya kwanza na bima ya afya.
(vii) Shilingi 20,000/= Mitihani ya kujipima mock
(viii) Karatasi bunda moja (ream1) kwa kila muhula.
(ix) Fedha ya tahadhari 10,000/= (haitarejeshwa)

**NB:** *Fedha hizo hapo juu zilipwe kwenye akaunti ya shule na tafadhali andika jina la mwanafunzi, kidato na tahasusi kwenye* ***pay in slip*** *na kuiwasilisha siku ya kuripoti shuleni***.**

**JINA LA AKAUNT: MLANGALI SECONDARY SCHOOL**
**NAMBA YA AKAUNT: 61201100051 NMB**

**Angalizo: Jumla ya ada na michango kwa wanafunzi ni shilingi 188,000/= (Laki Moja na Elfu THemanini na Nane tu) kwa mwaka**

**2.3. MAAGIZO MENGINE**

1. Ni marufuku mwanafunzi kumiliki simu au kukutwa na simu
2. Nimarufuku mwanafunzi kuvaa au kukutwa na mavazi ya nyumbani kinyume na maagizo
3. Nimarufuku mwanafunzi kutoka eneo la shule bila kibali
4. Mwanafunzi anapaswa kutambua malengo yaliyomleta shuleni na hivyo inabidi awe na NIDHAMU ya hali ya juu ili kukabili vyema masomo yake na kutimiza ndoto zake; Uongozi wa shule hautasita kumrejesha nyumbani mwanafunzi yoyote asiyefuata Ratiba,sheria na taratibu za shule.
5. Uje na fomu ya uchunguzi wa afya (Medical checkup) ikiwa imejazwa na daktari wa kituo Cha afya au Hospitali ya serikali.

   **FOMU HII YA MATIBABU IRUDISHWE SHULENI KWA MKUU WA SHULE WAKATI WA KURIPOTI.**

   **Tafadhali soma kwa makini maelezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.**

**2.4. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE.**

Shule ya sekondari Mlangali inaendeshwa kwa mujibu wa sheria za Elimu Na.25 ya mwaka 1978 . Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya Elimu nchini. Unatakiwa kuzingatia sheria na miongozo ifuatazo uwapo shuleni, ambazo zitafafanuliwa kwa maandishi na kupewa nakala yako mara baada ya kuripoti shuleni.

a) Unatakiwa kuheshimu viongozi wote wa serikali na shule, walimu, wafanayakazi wote, wananfunzi wenzako na jamii nzima kwa ujumla.

b) Unapaswa kuthamini na kuheshimu kazi zote utakazopangiwa za masomo na nje ya masomo kwa kuzingatia muda.

c) Hakikisha unahudhuria na kutimiza maandalizi yote ya jioni (Evening Preparation) kwa muda wote uwapo shuleni.

d) Hauruhusiwi kuwa nje ya eneo la shule bila kibali ama ruhusa maalum kutoka kwa Mkuu wa shule kwa shughuli yeyoyote ile. Zingatia mipaka ya eneo la shule kwa muda wote uwapo shuleni.

e) Ni lazima kuvaa sare za shule zilizopendekezwa na si vinginevyo kwa muda wote uwapo shuleni.

f) Utakuwa mlinzi wa kwanza mali zote za shule ikiwemo vifaa vya madarasani, miundombinu na mazingira yote ya shule.

g) Ni lazima kuzingatia ratiba yote ya shule kama ilivyopangwa ikiwemo kuhudhuria vipindi vyote vya masomo yako na shughuli zote za Elimu ya Kujitegemea.

h) Ni Marufuku kujihusisha na mahusiano ya kimapenzi na mwanafunzi mwenzako, wanakijiji ama mtumishi yeyoyote wa shule kwa kipindi chote uwapo shuleni.

i) Ni marufuku kumiliki ama kutumia simu ya mkononi na vifaa vingine vya mawasiliano uwapo shuleni. Huduma ya mawasilianao itaratibiwa na mkuu wa shule pamoja na mwalimu wa malezi.

**2.5 MAKOSA YATAKAYOSABABISHA MWANAFUNZI KUFUKUZWA SHULE.**

(i) Wizi

(ii) Kutohudhuria masomo kwa zaidi ya siku 90 bila taarifa / utoro

(iii) Kugoma na kuhamasisha mgomo

(iv) Kutoa lugha chafu kwa wanafunzi wenzake, walimu, walezi.

(v) Kupigana mwanafunzi kwa mwanafunzi, kumpiga mwalimu.

(vi) Wanafunzi wote wanatakiwa kuwa na nywele fupi wakati wote wawapo shuleni

(vii) Ulevi au unywaji wa pombe na matumizi ya madawa ya kulevya

(viii) Uasherati, uhusiano wa jinsia moja, kuolewa

(ix) Kusababisha ujauzito au kutoa mimba

(x) Kushiriki matendo ya uhalifu, siasa na matendo yoyote yale yanayovunja sheria za nchi

(xi) Kutembelea majumba ya starehe na nyumba za kulala wageni

(xii) Kumiliki, kukutwa au kutumia simu ya mkononi katika mazingira ya shule

(xiii) Kudharau Bendera ya Taifa

(xiv) Kufanya jaribio lolote la kujiua, au kutishia kujiua kama kunywa sumu n.k.

(xv) Uharibifu wa mali yeyote ya shule na ya umma kwa makusudi

(xvi) Kulala au kuwa nje ya eneo la shule bila ruhusa ya MKUU WA SHULE.

**NB: Hairuhusiwi mzazi/mlezi kumtembelea mwanafunzi (visiting)**

**KWA MAWASILIANO ZAIDI**

**MKUU WA SHULE: MWL. NESPER ABEL MDAPO**
**NAMBA YA SIMU: 0754 359 332**

**MAKAMU: MWL. THADEI ALBERTO NYIGO**
**NAMBA YA SIMU: 0756 346 564**

**KARIBU SANA MLANGALI SEKONDARI**

..........................................

HEADMASTER
MLANGALI SECONDARY SCHOOL
MBOZI

**MKUU WA SHULE**

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**PRESIDENT OFFICE**
**REGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT**

MLANGALI SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 535
MBOZI
DATE………………………..

MEDICAL OFFICER
GOVERNMENT HOSPITAL ……………
P.O. BOX …………………………………
…………………………………………….

<u>REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION</u>

Please examine ………………………………………………………………..(student name) as to her fitness for pursuing further Education at this school.

**…………………………**
**HEADMASTER**

1. Haemoglobin ……………………………………………………………………
2. P.V. Bleeding ……………………………………………………………………
3. Blood pressure …………………………………………………………………..
4. Blood Group ……………………………………………………………………
5. (a) Sight …………………………………………………………………………
   (b) Hearing ……………………………………………………………………...
6. Urine for sugar ………………………………………………..
7. Stool for routine – Examination …………………………………………………..
8. Athma ……………………………………………………………………………..
9. Skin diseases ……………………………………………………………………
10. Epilepsy …………………………………………………………………………
11. Leprosy …………………………………………………………………………..
12. Pulmonary tuberculosis …………………………………………………………
13. Deformity ………………………………………………………………………..
14. Mental problems ………………………………………………………………..
15. V.D. (Give type) ………………………………………………………………..
16. Any other serious disease note mentioned above …………………………………
    ……………………………………………………………………………………..

    **OTHER COMMENTS**: ……………………………………………………………
    …………………………………………………………….
    …………………………………………………………….
    …………………………………………………………….

**……………………………………..**

**DESIGNATION AND SIGNATURE**
**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

MKOA WA ……………………

OFISI YA MKUU WA WILAYA
WILAYA YA …………………
S.L.P. …………………………
……………………………

MKUU WA SHULE,
SHULE YA SEKONDARI MLANGALI
S.L.P. 535
MBOZI

**UTHIBITISHO WA URAIA WA TANZANIA.**

Nathibitisha kuwa ……………………………………………………………….. (Jina kamili la mwanafunzi ) ni raia wa Tanzania kwa kuzaliwa / kwa kuandikishwa.

Baba yake (Jina kamili) …………………………………………………………………
Amezaliwa katika Mkoa wa ………………………… Wilaya ……………………..
Tarafa ya ……………………….. kata ya …………………………………..

Mama yake (jina kamili) …………………………………………………………………
Amezaliwa katika kata ya ………………………………… Wilaya ya ……………………..
Mkoa wa ………………………………………………….

**………………………………**
**MKUU WA WILAYA**

**NB:** Kila **mwanafunzi analazimika kuishughulikia hati hii kikamilifu.**
**Ikisha jazwa irudishwe kwa mkuu wa shule siku ya kuripoti shuleni.**

**OFISI YA RAIS**
**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**
**SHULE YA SEKONDARI MLANGALI**
**FOMU YA AHADI MWANAFUNZI NA MZAZI / MLEZI**

**A. SEHEMU YA MWANAFUNZI:**

(a) Mimi ………………………………..nimezaliwa tarehe …………. Jina la Baba ………………………. Jina la Mama ……………………. Au jina la mlezi …………………………… nakubali kuingia kidato cha ……….. katika shule ya Sekondari MLANGALI kama mwanafunzi wa kutwa. Nitafika shuleni tarehe ……………………… bila kukosa au kuchelewa.

(b) Nitatii sheria zote za shule kama zinavyosomeka na nitaishi maisha mazuri ya mfano hapa shuleni. Nitakuwa mwanafunzi mwenye bidii katika masomo na kazi za kujitegemea. Sitakuwa mtoro shuleni. Wala kuwa mwanafunzi mwenye usumbufu wa aina yoyote ile . Naahidi kutoshiriki migomo ya aina yoyote ile hapa shuleni.

(c) Sahihi ya mwanafunzi………………………….. tarehe ………

**B. SEHEMU YA MZAZI/MLEZI:**

1. Mimi ……………………………….. ninakubali mtoto wangu (jina) ………………. ..Asome katika shule ya Sekondari Mlangali kuanzia tarehe …………………………………. Ninaamini kuwa Elimu ni urithi wa mtoto na **MWANGA WA MAISHA YAKE**
2. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote anayotakiwa kuwa nayo shuleni kama ulivyoagiza katika barua yako. Nitatoa na kutekeleza kwa wakati na bila usumbufu wowote.
3. ninaahidi kulipa karo ya shule pamoja na michango mingine kwa wakati inapohitajika. Vinginevyo nichukuliwe hatua kali, mimi Mzazi / Mlezi.
4. Ninakuhakikishia kwamba nitamwonya mtoto wangu kutii sheria za shule na kuishi maisha mazuri na ya mfano kwa wenzake. Nitamhimiza asiwe mtoro na msumbufu.
5. Ninakubali kuwa mtoto wangu amekubali kusoma katika shule ya Serikali ya Mlangali Sekondari kama mwanafunzi wa kutwana ataendelea hivyo hadi kumaliza kidato cha kwanza (1) Mimi sitamhamisha kwenda shule nyingine pasipo sababu.
6. Anuani yangu ya kudumu ni:-
   ………………………………………………………………..
   ………………………………………………………………..
7. Namba ya simu :……………………………………………
8. Sahihi : …………………………………….

**KWA MATUMIZI YA OFISI TU:**

Mwanafunzi ……………………………………………………………………amepokelewa tarehe : ……………………………………………………….. anamapungufu ya vifaa vifuatavyo:
1………………………………………….. 2. ………………………………………………………..
3………………………………………. 4. ……………………………………………………….

**SAHIHI: …………………………………………**

**MWALIMU ANAYEPOKEA**

## TAARIFA BINAFSI

1. Jina lako kamili kama lilivyotumika kidato cha nne ………………………………………
   Dini / dhehebu
   ……………………………………………………………………………
2. Jina kamili la baba mzazi / mlezi …………………………………………………………
   Kazi yake ………………………………………………………………………………
   Anwani kamili ya baba mzazi /mlezi …………………………………………………
   Namba ya simu ya mkononi …………………………………………………………
   Mahali anakoishi baba mzazi / mlezi. Mkoa ……………………..Wilaya ……………….
   Tarafa …………………………….. Kijiji / Mtaa …………………………………………
3. Jina kamili la mama mzazi / mlezi …………………………………………………
   Kazi yake ……………………………………………………………………………..
   Anwani kamili ya mama  mzazi / mlezi ……………………………………………...
   Namba yake ya simu ya mkononi …………………………………………………
   Mahali anakoishi mama / mlezi: Mkoa ……………………Wilaya ……………………
   Tarafa ……………………………………Kijiji / mtaa ……………………………
4. Taarifa ya ndungu wa karibu wanaoweza kushirikishwa kwenye malezi ya mwanafunzi awapo hapa shuleni.

| JINA KAMILI | UHUSIANO | MAHALI ANAPOISHI | ANWANI NA NAMBA YAKE YA SIMU | PICHA YAKE |
|---|---|---|---|---|
| 1. (BABA MZAZI) | | | | |
| 2.(MAMA MZAZI) | | | | |
| 1. (MLEZI) | | | | |
| 2.(MLEZI) | | | | |

NB: hawa ndio watawasiliana na uongozi wa shule kwa jambo lolote.

5. Shule nilizosoma msingi hadi kidato cha nne

| **JINA LA SHULE** | **DARASA/KIDATO** | **KUANZIA MWAKA HADI MWAKA** | **MKOA** | **WILAYA** | **KIJIJI** |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | | | | | |
| 2. | | | | | |
| 3. | | | | | |
| 4. | | | | | |
| | | | | | |

Matarajio yangu ya kumaliza kidato cha sita ni:

1. …………………………………………………………………………………………
2. …………………………………………………………………………………………
3. …………………………………………………………………………………………

6. Hapa shuelni ningependa nijiunge na :

1. Michezo (i) ………………………. (ii) ………………………. (iii) ………………………….
2. Kikundi cha utumaduni wa

   ……………………………………………………………………

3. Mradi wa ………………………………………………………………………………………

7. Mimi ………………………………………… wa kidato cha …………./ mchepuo …………………

   Mwaka …………………………………. Naahidi kuwa taarifa nilizotoa ni za kweli na zitumike wakati wowote zinapohitajika hapa shuleni.

   Saini ya mwanafunzi ……………………………………. Tarehe ………………………

8. Jina na sahihi ya mzazi / mlezi

   ………………………………………………………………

   Jina …………………………………………… Sahihi ………………………………

9. **Taarifa hii irudishwe kwa Mkuu wa Shule ya Sekondari Mlangali.**